



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA MKURANGA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MDC/S.20/20/VOL.V/32

17 Aprili, 2023

TANGAZO

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA ANAWATANGAZIA WATANZANIA WENYE SIFA KUOMBA NAFASI ZA KAZI YA DEREVA II KWA VIGEZO VILIVYOAINISHWA HAPA CHINI:

DEREVA DARAJA LA II - NAFASI MBILI (2)

A. SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na cheti cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha IV na Leseni ya udereva daraja la E au C1 ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
2. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachombuliwa na Serikali.
3. Mwombaji mwenye cheti cha majaribio ya ufundi atafikiriwa kwanza.
4. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
5. Awe amesajiliwa na Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA) mwenye kadi au namba ya usajili.

B. MSHAHARA:

Waombaji watakapata nafasi ya kuajiriwa kwa cheo cha dereva II watalipwa mshahara katika ngazi ya mshahara ya TGS B.

C. MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA II

- 1) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- 2) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- 3) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- 4) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- 5) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- 6) Kufanya usafi wa gari, na
- 7) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, S.L.P 10, Mkuranga, Simu: +255 232-402738, Nukushi: +255 232402706, Barua pepe: ded@mkurangadc.go.tz, Tovuti: www.mkurangadc.go.tz

A. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:

Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na Nakala ya vyeti vya Elimu na Taaluma zilizothibitishwa, Wasifu wa Muombaji (CV), Nakala ya Kitambulisho cha NIDA au Namba ya NIDA iandikwe kwenye Wasifu wa Mwombaji, picha mbili "Passport size" na namba za simu zitumwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 10,
MKURANGA.

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 30/04/2023 SAA 9:30
ALASIRI.**

Limetolewa na;



Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
MKURANGA